HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

E- mail: uchilesekondari@yahoo.com
Mob: +255 (0) 752 476 389

P.O. BOX 582
SUMBAWANGA

KUMB. NA. USS/JOINING/F.V/04

10 Juni 2018

…….....……
……
…….……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UCHILE WILAYA YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA 2018/2019.

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Uchile mwaka 2018 kwa mchepuo wa **HGK/CBG** . Shule ipo katika mji mdogo wa Laela umbali wa kilometa 88 kutoka Sumbawanga Mjini kufuata barabara ya kwenda Mbeya, Upo usafiri wa mabasi kila siku, Unaweza kupanda magari yaendayo Mbeya na kushuka Laela au panda magari yanayoishia Laela. Nauli ni Tsh. 5,000/= toka Sumbawanga Mjini. Kama unatoka Mbeya kwenda sumbawanga shuka Laela, shule ipo Kilomita moja upande wa mashariki kutoka stand ya mabasi Laela.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 02/07/2018 mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/07/2018. Aidha, hakuna mwanafunzi atayepokelewa baada ya tarehe hiyo.

1:0 MAAGIZO MUHIMU YA KUZINGATIA

1:1 SARE YA SHULE

i. Sketi Mbili. Moja rangi ya khaki na nyingine ya damu ya mzee mshono wa kawaida ndefu mpaka chini
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
iii. Tai mbili. moja rangi ya khaki na nyingine ya damu ya mzee
iv. Viatu vya kamba jozi mbili rangi nyeusi
v. Soksi nyeupe
vi. Sweta rangi ya bluu
vii. T-shirt nyeusi yenye kora nyeupe.
viii. Raba pamoja na trucksuit light blue kwa ajili ya michezo.
ix. Gauni lefu yenye kitambaa cha draft ya bluu na nyeupe ambalo litavaliwa baada ya vipindi vya darasani (shamba dress).

MUHIMU: Kwa waislamu njoo na hijab yenye rangi nyeupe itakayovaliwa sambamba na sare ya shule.Aidha, mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani tofauti na maelekezo.

2:3 ADA NA MICHANGO YA SHULE.

a) Ada ya shule ni **Tsh 70,000/=** kwa mwaka, unaweza kutoa **Tsh. 35,000/=** kwa kila muhula.

b) Michango muhimu inayotakiwa kulipwa na kila mzazi.

i. Tahadhari sh. 5,000/=
ii. Kitambulisho na picha shilingi. 6,000/=
iii. Nembo ya shule shilingi 2,000/=
iv. Mchango wa Taaluma shilingi.20,000/=
v. Ukatarabati wa samani shilingi. 20,000/=
vi. Mchango wa mpishi,ulinzi na vibarua wengine shilingi. 30,000**/=**
vii. Huduma ya kwanza shilingi. 10,000/=
viii. Mtihani wa mock shilingi 20,000/= (fedha hii ilipwe muhula wa kwanza kidato cha sita)

NB. Fedha zote za michango ziwekwe kupitia Benki NMB Sumbawanga kwa akaunti za shule zifuatazo:

AINA YA MCHANGO	**NAMBA YA AKAUNTI**	**JINA LA BENKI**	**JINA LA AKAUNTI**
Ada ya Shule	**62101100106**	NMB	Uchile Secondary School Revenue Collection Account
Michango mingine	**62110007595**	NMB	Uchile Secondary School E.K Account

C. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO KILA MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.

i. Godoro la ft 21/2
ii. Aje na madaftari ya kutosha
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa biolojia
iv. Scientific calculator
v. Aje na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi
vi. Shuka mbili rangi ya bluu na blanketi moja kwa ajili ya kujikinga na baridi.
vii. Chandarua
viii. Kijiko, sahani, bakuri na kikombe kwa ajili ya chakula.
ix. Aje na vifaa vya usafi binafsi kama ndoo n.k
x. Ream ya karatasi 1(A4) kwa mwaka
xi. Jalada 1
xii. Kila mwanafunzi aje na vifaa vya usafi yaani Jembe lenye mpini, Fyekeo, Fagio, ndoo yenye ujazo wa lita 20,Mopa, dryer na ndoo yake

MUHIMU: Kila mwanafunzi anapokuja kuripoti ni lazima aje na **Original Result Slip** na **Leaving Certificate.**

3:0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

3:1. Shule ya Sekondari Uchile inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli utakazopewa ndani na nje ya shule
iii. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation)
iv. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

3:2 ***MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.***

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, n.k
v. Kupigana au kupiga
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kupata ujauzito au kutoa mimba
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
xiii. Kutohudhuria masomo kwa muda wa siku 90 bila taarifa
xiv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
xv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

N:B Mwanafunzi atajaza fomu maalumu ya kutii na kufuata sheria na kanuni za shule mara atakaporipoti shuleni.

Muhimu: Mwanafunzi atapokelewa iwapo atakuwa amekamilisha michango yote ya shule na kujaza fomu zote zilizoambatishwa na barua hii

"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI UCHILE"

W.J. LUCAS
MKUU WA SHULE.

SHULE YA SEKONDARI UCHILE

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi …… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo, nakubali kujiunga na shule ya Sekondari Uchile. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Sekondari Uchile na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi……..Tarehe……

Mimi……..(Jina la mzazi/mlezi) Nimeshuhudia mtoto wangu ……..(Jina la mwanafunzi) akikubali kwa hiari kujiunga na shule ya sekondari Uchile, ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea mtoto wangu naamini tutakuwa tunawasiliana katika kuhakikisha mwanafunzi anafanya vizuri katika masomo yake.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……Tarehe……..

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

UCHILE HIGH SCHOOL
P.O. BOX 582
SUMBAWANGA.

DATE……

MEDICAL OFFICER
……
……
……
……

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR…… (NAME OF STUDENT)

Please examine the above named as to his/her fitness as indicated below. Arrange the necessary treatment so that the certificate may be brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a recognized Government hospital.

1. Hemoglobin ……
2. P.v Blooding ……..
3. (a) Blooding ……...
   (b) Hearing …….
4. Blood pressure ……...
5. Stool for routine examination ……...
6. Urine for sugar ……...
7. Skin diseases ……..
8. Leprosy …….
9. Pulmonary tuberculosis ……
10. Asthma …….
11. Epilepsy ……..
12. Deformity ……
13. Mental problem ……
14. Comment……..……. ……
    …..…….……

Name of medical officer……. Signature……. Date……

Official stamp